TANGAZO LA SERIKALI Na.....…….. la tarehe …….

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1)(z) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA, 2017

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru na Huduma) za Halmashauri ya Wilaya Mtwara za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Mtwara

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni ya Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya Mtwara

"Hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo ya bidhaa, kazi au Huduma katika mwaka wa fedha.

Sura 212

"Kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni

Sheria Na.7 ya mwaka 2011

"Kazi" maana yake ni kama ilivyotafsiliwa kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma.

"Kipindi Maalum cha Hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mtwara pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Taasisi ya biashara" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa inayofanya biashara, kazi au kutoa huduma kwa lengo la

kupata faida.

"Tawi la Kampuni" ni tawi la kampuni iliyosajiriwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.

"Ushuru wa Huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa Kampuni, Tawi la kampuni, Taasisi ya biashara, au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya Umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri.

"Ukokotoaji" maana yake ni namna ya kuandaa kiasi cha Ushuru wa Huduma kitakacholipwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa Ushuru wa Huduma

4. Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kwa kampuni, taasisi ya biashara au tawi la kampuni au manyabiashara yoyote kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika ndani ya eneo la halmashauri.

Wajibu wa kulipa Ushuru wa Huduma

5. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara, kampuni, taasisi ya biashara au tawi la kampuni kulipa Ushuru wa Huduma utokanao na utoaji wa huduma , kazi, mauzo ya bidhaa katika eneo la Halmashauri;

(2) Manyabiashara, atawasilisha kwa halmashauri taarifa za hesabu za mauzo kwa kila mwezi husika na atalipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa viwango vitakavyotokana na hesabu hizo au viwango vilivyotajwa na sheria ndogo hizi kwa mfanyabiashara asiye na vitabu vya biashara.

(3) Endapo mfanyabiashara, kampuni, taasisi ya biashara au tawi la kampuni itashindwa kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo kwa wakati, Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumtaka Mfanyabiashara yoyote kuwasilisha taarifa hizo ndani ya siku thelathini zinazohusu kipindi maalum cha hesabu zikionyesha kiasi na thamani ya fedha za mauzo ya bidhaa zilizoingizwa, kusambazwa au kuuzwa, na kazi, au huduma zilizotolewa.

(4) Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu taasisi yoyote ya mfanyabiashara yoyote anayepaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumiwa kama taarifa sahihi.

(5) Endapo Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kwa uzembe au makusudi atasababisha hasara katika kutekeleza majukumu

aliyopewa katika Sheria Ndogo hizi Halmashauri itawajibika kulipa fidia kwa hasara iliyojitokeza

Namna ya kukusanya Ushuru wa Huduma

6. (1) Halmashauri itakusanya Ushuru wa huduma kiwango kisichozidi Asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mapato halisi baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya mlaji, kutoka kwa kampuni, tawi ya kampuni, taasisi za biashara,au mtu yeyote anaewasilisha hesabu za mauzo kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (**1**) cha kifungu cha **6** mfanyabiashara ambaye hawasilishi hesabu zake Mamlaka ya Mapato Tanzania atalipa ushuru wa huduma kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi.

(3) Ushuru wa huduma unaweza kulipwa kwa mwezi, miezi mitatu (robo mwaka) au kwa mwaka.

Ukokotoaji Ushuru wa Huduma

7. (1) Halmashauri kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi itakokotoa na kutoza Ushuru wa Huduma.

(2) Ushuru uliokokotolewa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi utalipwa ndani ya kipindi cha siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya kupata taarifa ya ukokotoaji.

Makosa

8. Itakuwa ni kosa kwa kampuni au tawi la kampuni , taasisi ya biashara, mfanyabiashara au mtu yeyote :-

(1) Kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi ndani ya muda ulioainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Kuwasilisha taarifa zisizo sahihi.

(3) Kutolipa Ushuru wa Huduma.

(4) Kutolipa kwa wakati Ushuru wa Huduma ndani ya muda uliowekwa na Sheria Ndogo hizi.

(5) atashawishi kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kukataa au kukwepa kulipa Ushuru wa Huduma.

(6) Atamzuia mtumishi wa Halmashauri kutekeleza majukumu aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

9. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kiasi kisichozidi shilingi laki tatu (Tsh.30 0,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum

iliyoambatishwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kulipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

10. Mtu yeyote atakatekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 6(2)

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa Huduma

Na.	**Aina ya biashara**	**Kiasi cha Ushuru**	**Muda**
		20,000/=	Kwa mwaka
1.	Saloon	20,000/=	Kwa mwaka
2.	Gereji na Karakana	20,000/=	Kwa mwaka
3.	Duka la jumla	20,000/=	Kwa mwaka
4.	Duka la rejareja	20,000/=	Kwa mwaka
5.	Bucha	20,000/=	Kwa mwaka
6.	Stationary	20,000/=	Kwa mwaka
7.	Bar	20,000/=	Kwa mwaka
8.	Grosary	20,000/=	Kwa mwaka
9.	Biashara na huduma zinginezo	20,000/=	Kwa mwaka

JEDWALI LA PILI
KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa Chini ya kifungu cha 9

Mimi ……wa S.L.P…….…….. nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya…….…..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mtwara kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi….Mwaka……nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……..cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya Mtwara za mwaka 2017.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mtwara. Niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru wa Huduma ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya mwezi……mwaka……

Jina……..……...Saini…….....

Mbele ya:

Jina……..…….

Saini…….….

Wadhifa……